# Mtume Muhammad ni nabii wa rehema

**Prof. Muhammed Mukhtar Jumaa**

**Waziri wa Wakfu**

Mwenyezi Mungu Mtukufu amemleta Mtume Muhammad (rehma na amani zimshukie) kuwa ni rehema kwa ulimwengu mzima, akasema: {na wala hatujakutuma isipokuwa ni rehema kwa ulimwengu mzima} na Mtume akajieleza mwenyewe kwa kusema “enyi watu hakika mimi ni rehema yenye kuongoa.” Na Qur’ani Tukufu inasisitiza kuhusu hilo na kusema { Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma. }

Na kitabu chake alichoteremshiwa Mtume ni kitabu chenye uongofu kwani Mweneyzi Mungu anasema **{**Na tunateremsha katika Qur'ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhaalimu ila khasara}

Dini yake ni dini ya rehema,amani na usalama kwa viumbe wote, dini yenye misingi thabiti ya kuwawezesha watu wote waishi kwa amani. Inahifadhi kutomwaga damu, inahifadhi mali zote kwa misingi ya kiutu bila ya kutafautisha watu kwa misingi ya dini, rangi, jinsia na kabila, nafsi zote zimehifadhiwa, heshima na mali pia zimehifadhiwa.  Na amana zote hurejeshwa kwa weneywe bila ya pingamizi. Na Mtume wetu (rehma na amani zimshukie) wakati wa kuhamia

kwake Madina alimuacha Ali bin Abi Twalib nchini Makka ili azirudishe amana kwa watu wake ingawa walimnyanyasa na kumkera.

Na siku walipokuwa mji wa Taifu watu wa mji ule walipowaamuru watumwa na watoto wamrembee kwa mawe mpaka akamwagika damu nyingi miguuni mwake, wakamjia malaika wa majabali na kumwambia : "Ewe Muhammad hakika Mweneyzi Mungu amesikia maneno ya watu wako kuhusu wewe na mimi ni malaika wa majabali Mwenyezi Mungu amenituka kwako ili uniamrishe kwa amri yako pindi ukitaka niwagandamize katika majabali mawili. Mtume (rehma na amani zimshukie) akasema: "lakini ninaema,ewe Mweneyzi Mungu waongoe watu wangu kwani hawajui walitendalo, nami ninataraji kuwa Mwenyezi Mungu atatoa katika migongo yao atakaesema Lailaha illa llahu (hapana wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mweneyzi mungu)."  Na alipoambiwa. "Waombee washirikina" akasema: mimi sikutumwa kuwa ni mweneye kulaani lakini nimetumwa kuwa ni rehema.

Uisilamu ni dini ya rehema na amani wa ulimwengu wote, hakuna mauaji kwa sababu ya itikadi hata kidogo, na Mtume (rehma na amani zimshukie) alipomuona mwanamke wa kikafiri ameuliwa katika uwanja wa vita akasema: "ni nani amemuua? Huyu haikupasa kuuliwa." Hii inathibitisha kuwa ukafiri si sababu ya kuuliwa, isipokuwa mauaji hutokea kwa sababu ya kuondoa uadui kwani dini hailazimishi mtu na wala haina maneno ya kejeli, Mweneyzi Mungu anasema kumwambia Mtume wake { . Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe, na waombee maghfira, na shauriana nao katika mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao mtegemea.} na Qur'ani ilipowazungumzia makafiri kupitia ulimi wa Mtume (rehma na amani zimshukie)

na kwa ndimi za masahaba wake akasema { Na hakika sisi au nyinyi bila ya shaka tuko kwenye uwongofu au upotofu ulio wazi.} na wala hakusema “sisi tupo katika uongofu na nyinyi mupo katika upotevu wa wazi, na misemo kama hii inajulikana kwa wasomi wa ufasihi wa maneno kuwa ni “ kunyeyekea”. Na hii ndio tamaduni yetu ambayo inamfanyia uadilifu mwengine hata katika kuzungumza.

Uisilamu umeamrisha kusema maneno mazuri, mwenyezi Mungu akasema Semeni na watu vizuri} na watu inakusudiwa kwa ujumla pia semeni maneno mazuri {na sema kuwaambia waja wangu waseme maneno ambayo ni mazuri} na watende pia vitendo vyema. { Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu} huyu ndiye Mtume wetu na hizi ndizo tabia zake akasema “nimetumwa kukamilisha tabia njema”

Na iwapo dini yetu ni dini ya rehema na kitabu chetu ni kitabu cha rehema na Mtume wetu (rehma na amani zimshukie) ni wa rehema sasa vipi kuhusu sisi? Tumefikwa na nini? Na ni kipi kilichowafika wenye nyoyo dhaifu juu ya dini yetu hata wakafikia kuwa wana nyoyo ngumu kiasi hiki? Na utatuzi wake ni upi**?**

Hapana shaka kuwa vitendea kazi vingi vinahusika juu ya hili, ikiwemo wasomi wasio na fani husika kuwa na mamlaka katika kutoa hutuba za ulinganio na kushika nafasi hizo kwa muda mkubwa. Na wengine kuamisi sivyo na kuzidisha itikadi kali katika dini, yote haya ni ufahamu usio sahihi na ipo haja ya kusahihisha pamoja na kusisitiza kuwa uisilamu ni dini ya msamaha, rehema na wepesi. Na wasomi wamesema kuwa “Fiqhi” ni utambuzi na uwepesishaji kwa dalili, na hakuna aliyesema yeyote katika wenye kutegemewa elimu zao sawa katika wale wa zamani au wa somi wa kisasa kuwa “fiqhi” ni elimu yenye itikadi kali. Mweneyzi Mungu anasema { Mweneyzi Mungu anakutakieni wepesi wala

hakutakieni uzito} na anasema {Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini. Nayo ni mila ya baba yenu Ibrahim. Yeye (Mwenyezi Mungu) alikuiteni Waislamu tangu zamani, na katika hii (Qur'ani) pia, ili awe Mtume shahidi juu yenu, na nyinyi muwe mashahidi kwa watu}. Pia anaendelea kusema {Na jueni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko nanyi. Lau angeli kut'iini katika mambo mengi, bila ya shaka mngeli taabika. Lakini Mwenyezi Mungu amekupendezeeni Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na amekufanyeni muuchukie ukafiri, na upotovu, na uasi. Hao ndio walio ongoka, 8. Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na neema zake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima. }. Na Mtume wetu (rehema na amani zimshukie) hakuwa akichagua kati ya mambo mawili isipokuwa akichagua lililo jepesi lao ilivyokuwa si katika maasi au kuvunja undugu, na Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa ni mwenye kujiepusha sana katika maasi